

**Issue no:** 01 | **Vol no:** 07 | **February** 2026: 01-12

# Athari za Nyimbo za Kilimo katika Jamii ya Wasukuma katika Jamii za Leo

**Olivia Kanwa**

**Bishop Stuart University, Uganda.**
Author's email: kanwaolivia@yahoo.com

**Article History**
Received: **2025.12.19**
Accepted: **2026.01.14**
Published: **2026.02.27**

**Cite this article in APA**
Kanwa, O. (2026). Athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma katika jamii za leo. *Editon consortium journal of Kiswahili* , *7*(1), 01-12. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.662

**Ikisiri**
Makala hii inahusu athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma kwa kujikita katika wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza, katika muktadha wa jamii ya leo. Kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, kumekuwa na hofu kuwa nyimbo za kilimo hazina umuhimu katika jamii ya sasa. Hivyo, makala hii inalenga kuweka bayana umuhimu wa nyimbo hizo katika jamii ya leo. Utafiti huu umetumia nadharia ya Usosholojia wa Fasihi iliyomwongoza mtafiti katika ukusanyaji na uchambuzi wa nyimbo za kilimo. Aidha, nadharia ya Utendaji wa Maigizo imemwezesha mtafiti kutambua namna nyimbo hizo zinavyotekelezwa miongoni mwa hadhira na kuainisha tabia zao. Usampulishaji wa makusudi ulitumika katika kuchagua vikundi vya kilimo vilivyosajiliwa katika kata, vyenye jumla ya watu themanini (80), na mbinu ya usampulishaji wa kubahatisha ilitumika kupata sampuli iliyosaidia kutoa taarifa zilizohitajika kuhusu athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za mahojiano, hojaji, ushiriki na ushuhudiaji. Vifaa kama kamera, kinasa sauti, redio na kanda vilitumika katika ukusanyaji wa data hizo. Kupitia mbinu hizo, mtafiti aliweza kukusanya data zilizohitajika na kukidhi malengo ya utafiti. Katika lengo la kwanza, nyimbo zilizobainishwa ni pamoja na nyimbo za kupanda, kupalilia na kuvuna. Lengo la pili lilihusu kubainisha dhima za nyimbo hizo, zikiwamo kuhamasisha jamii katika kazi, kukuza talanta na sanaa, kuburudisha jamii, kukuza ushirikiano miongoni mwa wanajamii, kuonyesha hisia za mtu binafsi, pamoja na kuendeleza na kueneza utamaduni wa jamii husika. Lengo la tatu lilihusu kutoa mapendekezo, ambapo ilipendekezwa kuwa nyimbo za jamii ya Wasukuma zihifadhiwe katika machapisho na mitandao mbalimbali ili ziweze kuonwa na vijana wa sasa na kuthaminiwa kama ilivyokuwa hapo awali miongoni mwa wanajamii.

**Maneno muhimu:** Athari, nyimbo, jamii, kilimo, utamaduni.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## 1.0 UTANGULIZI

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, jamii za Wasukuma zimekumbwa na hofu kuwa nyimbo za kilimo zimepoteza umuhimu katika jamii ya leo. Hii ni kutokana na kutotumiwa mara nyingi miongoni mwa wanajamii kama ilivyokuwa awali. Utafiti huu unalenga kuweka bayana namna nyimbo hizo ambazo bado zina umuhimu katika jamii ya leo, kwa sababu kilimo bado kipo na kitaendelea kuwepo.

Wasukuma ni kabila kubwa sana nchini Tanzania ambalo linakadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni sita. Kabila hili huishi katika eneo la Kaskazini Magharibi mwa Tanzania, karibu na mwambao wa Kusini mwa Ziwa Victoria, ambapo kuna mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita na Shinyanga. Baadhi ya Wasukuma wapo mkoani Tabora. Shughuli zao kuu za kiuchumi ni kilimo, uvuvi, ufugaji na biashara. Pamba ndiyo zao kuu la kibiashara kwa Wasukuma. Wanafanya pia shughuli za uchimbaji na uuzaji wa madini mbalimbali kama vile dhahabu, almasi na madini mengineyo ambayo huchimbwa katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Mwanza, Geita na Shinyanga. Wasukuma wanashughulika sana na kilimo cha mazao ya nafaka na ufugaji wa mifugo ya aina mbalimbali. Katika maeneo ya Shinyanga wanalima mazao ya nafaka kama mahindi na mpunga zaidi kuliko mazao mengineyo.

Wasukuma wa mikoa mingine hujishughulisha zaidi na kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula kama vile mpunga, mhogo, mahindi na viazi vitamu, pamoja na mazao ya biashara kama pamba na alizeti kwa kiasi. Chakula kikuu cha Wasukuma ni ugali pamoja na maziwa kwa kuwa familia nyingi hujihusisha na ufugaji wa ng’ombe. Wasukuma huwasiliana kwa lugha yao inayojulikana kama Shisukuma (Kisukuma), japo katika makala hii limetumika zaidi neno Kisukuma au Wasukuma. Lugha hii hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi ili kudumisha na kuendeleza lugha yao (Masanja 2019).

Mfumo wa maisha katika jamii za Wasukuma ni mfumo jike, ikimaanisha kuwa mwanamke ndiye mlezi na mtawala wa familia, na baba kazi yake ni kuzalisha na kutafuta kipato kitakachoweza kuiendesha familia. Kwa mujibu wa watafitiwa, wanawake hawa walitoka sehemu na makabila mbalimbali ambao walifika katika eneo husika kwa malengo tofauti. Suala hili huifanya jamii ya Wasukuma kuwapenda na kuwathamini wanawake, wakiamini kuwa ni walezi na watunzaji wa familia kwa maana wametoka koo mbalimbali tofauti na wanaume. Jamii za Wasukuma hujishughulisha na shughuli mbalimbali kama vile za kiuchumi, kisiasa, kitaaluma, kijamii na kiutamaduni. Wasukuma ni jamii yenye mchanganyiko wa imani ambazo wamezihifadhi na kuziendeleza kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo. Imani hizo zimeendelea kuhifadhiwa kupitia sanaa, mila na desturi, zikiwamo ngoma ambazo zinaambatana na nyimbo mbalimbali. Miongoni mwa nyimbo hizo ni nyimbo za kilimo. Nyimbo za kilimo ni miongoni mwa nyimbo kongwe katika jamii ya Wasukuma (Budebah 2014).

Kutokana na utamaduni wao, Wasukuma wana desturi ya kuimba nyimbo wakati wa kulima (wanaume) na katika shughuli nyinginezo kama kusaga na kutwanga (wanawake). Hili ndilo jambo lililoshughulikiwa na makala hii katika kuchunguza athari za nyimbo hizo katika jamii za sasa za Wasukuma.

### 1.1 Usuli wa Nyimbo

Kuvuna (2013) anaeleza kuwa nyimbo ni kipera katika utanzu wa ushairi. Mojawapo ya malengo ya elimu ni kutambua, kudadisi, kudhamini na kustawisha aina mbalimbali za tanzu za lugha na fasihi kwa jumla. Kwa hivyo, utafiti wa nyimbo za kazi katika jamii ya Warabai utakidhi lengo hili. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), nyimbo zina historia ndefu katika jamii zetu. Anasema nyimbo zilianza mara tu binadamu alipopata lugha na kuweza kuzieleza na kuzifumbata hisia zake. Kipera cha nyimbo kimefasiriwa kwa njia mbalimbali. King’ei na Kisovi (2005) wanaeleza wimbo kama utungo ambao una mpangilio maalum wa maneno na una mahadhi. Huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi.

TUKI (2004) wanafafanua wimbo kuwa ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Wamitila (2003) amefafanua nyimbo kuwa ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki. Mulokozi (2017) anaeleza kuwa wimbo ni kila kinachoimbwa. Hata baadhi ya tanzu za kinathari kama vile hadithi zinazoimbwa huingia katika kundi hili la nyimbo, ambazo ni:

a. Muziki wa sauti ya mwimbaji
b. Muziki wa ala (kama ipo)
c. Matini au maneno yanayoimbwa
d. Hadhira inayoimbiwa

e. Muktadha unaofungamana na wimbo huo, mfano sherehe, ibada, msiba na kilimo

Kulingana na wataalamu na watafiti mbalimbali wa fasihi simulizi kama Finnegan (1977), wanaeleza kuwa nyimbo zilianza pale tu binadamu alipoanza kupambana na mazingira yake katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Hivyo, utanzu huu wa nyimbo kama kipera cha ushairi katika tanzu za fasihi simulizi ni kongwe ukilinganisha na tanzu nyingine za fasihi simulizi.

Finnegan (1970) anathibitisha wazo hili kwa kusema kuwa shughuli nyingi za binadamu kama vile harusi, tohara, mazishi, kulima na kuvuna hushirikisha nyimbo. Miongoni mwa majukumu ya nyimbo ni kuhimiza wafanyao kazi kujitahidi na kuendelea kufanya kazi bila ulegevu na pia kuleta umoja.

Nyimbo zimechipuka kutoka ushairi simulizi wa Kiswahili, na ndiyo maana ni vigumu kuzungumzia nyimbo bila kuugusia ushairi. Miruko (2016) anasema ushairi (nyimbo) ni maneno yanayoeleza hisia nzito za binadamu, fikra na mawazo yanayopangwa kwa mpango maalumu uitwao beti. Kimantiki, nyimbo haziwezi kumalizika kwenye mpangilio mzuri wa maneno tu, bali ni sanaa ya lugha; lazima maneno yanapoelezea hisia na fikra yawe mateule yaliyofinyangwa na kusukwa kwa nidhamu maalumu inayompendezesha muimbaji na kumfurahisha msikilizaji.

Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutoa maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno yanayotamkwa au kutendwa, yaani husimuliwa kwa njia ya mdomo na kwa vitendo. Kipengele cha lugha ni muhimu sana katika fasihi hii kwa maana ndicho hutofautisha fasihi simulizi na sanaa nyinginezo. King’ei na Kisovi (2005) wanaieleza fasihi simulizi kuwa ni sanaa ya mazungumzo ya kubuni yanayosimuliwa, kukaririwa, kuigizwa au kuhadithiwa.

Ravindra (1971) na Makoye (2010) wanafafanua kuwa Wasukuma wanapenda kuimba na kucheza katika shughuli zao za kilimo, kusaga na kutwanga nafaka zao, ambapo kazi hizo huambatana na kuimba nyimbo mbalimbali. Katika jamii za Wasukuma, ngoma na nyimbo huambatana kwa wakati mmoja, kwa maana wakati kimoja kinafanyika kingine hufanyika sambamba nacho. Ni mara chache sana kukuta Wasukuma wanafanya kazi yoyote bila kuambatana na uimbaji wa nyimbo.

Kwa hiyo, nyimbo katika jamii za Wasukuma zilianzishwa kama silaha ya kazi kwa kuwatia hamasa katika kazi. Vilevile, ziliwafanya wanaume ambao ndiyo vielelezo vya kazi katika jamii ya Wasukuma wasidhalilike mbele ya wanawake kwa kushindwa kufanya kazi. Nyimbo zilikuwa zikitumika katika kazi zote za nguvu kama vile kuvuta kokoro (kwa wavuvi), kuchimba mashimo kwa wachimba madini pamoja na kilimo. Dhima zimekuwa zikipanuka kadri jamii inavyobadilika na kupanua wigo wa nyimbo hizo za kilimo (Masanja, 2019).

Nyimbo za kilimo ni kongwe kama kazi za kilimo zilivyo, na huimbwa wakati wa kufanya kazi za kilimo kama kuandaa shamba, kupanda, kupalilia na kuvuna. Nyimbo hizo huwa na athari mbalimbali kwa jamii hizo, jambo ambalo limeshughulikiwa na utafiti huu.

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Watafiti mbalimbali wamefanya utafiti juu ya nyimbo za asili, akiwemo Mulokozi, M.M., ambaye amechambua nyimbo za nyiso kutoka Zanzibar (1939). Kavugha (1977) alichunguza mila na desturi za Wapare. Josphat na wenzake (2022) wametafiti maudhui katika nyimbo za tohara zilizodenguliwa na nyimbo za dini za Kiigembe katika kuafikia maendeleo endelevu kwa Waigembe. Asajile na wenzake (2025) walifanya utafiti wa maadili katika nyimbo za harusi katika kabila la Wanyakyusa. Pia Kadallah (2018) ametafiti utendaji katika nyimbo za Wasambaa. Budebah (2014) ametafiti mbinu za utunzi wa nyimbo ndefu katika ngoma ya Wigashe. Sim (Kiango, 1995) na Mbijima (2023) wametafiti kuhusu nyimbo za jando na unyago.

Licha ya kuwa wataalamu hawa wameshughulikia suala la nyimbo katika jamii mbalimbali, mtafiti amebaini tatizo kwamba nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma hazijaingizwa katika maandishi vya kutosha, bali zimetafitiwa kijumla kama nyimbo za kazi na Makoye (2005, 2010) pamoja na Masanja (2019), ambao hawajatafiti kabisa suala la athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma, hususani wilaya ya Kwimba. Kwa hiyo, zikifanyiwa utafiti zitaingizwa katika maandishi na baadaye zitakuwa hazina kubwa kwa kizazi kilichopo, kijacho na Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo basi, utafiti huu utaweza kutatua tatizo hilo na kuziba pengo la utafiti kuhusu athari za nyimbo za kilimo katika jamii za Wasukuma.

## 2.0 MAPITIO YA MAANDISHI

### 2.1 Mapitio ya Maandishi Kuhusu Nyimbo za Kilimo kwa Ujumla

Sehemu hii imepitia mawazo mbalimbali ya wataalamu walioandika kuhusu nyimbo za kilimo kama sehemu mojawapo ya mila na desturi, na nyimbo kama sehemu mojawapo ya utanzu wa fasihi simulizi. Kilimo kama sehemu ya shughuli za kijamii na kiuchumi kimeangaziwa kwa undani na wataalamu mbalimbali.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa nyimbo ni tanzu mojawapo ya ushairi ambayo huwa na mizani kwa ajili ya kuimbika kulingana na lengo la mtunzi. Anaendelea kusema kuwa wimbo ni kazi ya sanaa ambayo hutoa wazo au tukio kwa namna inayovuta hisia kutokana na mpangilio maalumu wa maneno unaoleta mvuto wakati wa kuusoma au kuuimba wimbo huo.

Wamitila (2004) anafasiri nyimbo kuwa ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka, huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Anafafanua zaidi kwamba nyimbo huchukua sehemu kubwa ya miviga (sherehe) ya jamii mbalimbali. Hoja ya nyimbo kuhusishwa na sherehe pamoja na shughuli mbalimbali za kijamii imejadiliwa pia na Simiyu (2007), ambaye amefasili nyimbo kwa kujikita katika maana na namna zinavyotumika katika jamii.

Wamitila (2003, 2004) na Simiyu (2007) wamesaidia kueleza maana ya nyimbo na matukio yanamoimbwa, ila fasili zao hazijaeleza kuhusu nyimbo za kilimo, ambalo ndilo jambo lililoshughulikiwa na makala hii katika jamii ya Wasukuma.

Ng'ata (2023) anafasili wimbo kuwa ni utungo ulio na mdundo na mahadhi na unaoweza kuimbika. Nyimbo ni maarufu sana katika jamii nyingi za Afrika zinazoandamana na dansi na ngoma. Ufafanuzi wa mtaalamu huyu umesaidia kuelewa maana ya nyimbo, ila haujagusia nyimbo za kilimo; pengo hili limezibwa na utafiti huu.

Mwangosi (2017) anaeleza kuwa nyimbo za Magosi zinatazamwa kama muziki mbadala wa kizazi kipya unaofuata kaida za mkondo wa kijadi katika kuhakiki mifumo ya kijamii kwa jicho pevu. Upokezi na ukuaji wake, kama ilivyo kwa muziki wa kizazi kipya ulioshika kasi kuanzia miaka ya 1990 na 2000 nchini Tanzania (Suriano, 2006 na Omary, 2009), ndivyo ilivyo kwa upande wa nyimbo za Magosi kuanzia miaka ya 2000. Mwangosi anazungumzia nyimbo za Magosi zinazohusu jamii ya Wanyakyusa wa Mbeya, ila hali hii pia imejitokeza katika jamii ya Wasukuma kuhusu nyimbo za kilimo. Vijana wanatumia sana nyimbo za kilimo zenye mapigo ya muziki wa kizazi kipya unaopendwa na vijana wa leo. Usukumani, nyimbo hizo za kilimo zinashika kasi miongoni mwa vijana wa sasa tofauti na ilivyokuwa awali.

Mtafiti huyu amesaidia sana katika kuelewa mabadiliko ya nyimbo kulingana na wakati pamoja na nafasi yake katika jamii ya Wanyakyusa, ingawa hajazungumzia nyimbo za kilimo ambalo ndilo lengo kuu la makala hii.

Budebah (2014) anaeleza kuwa nyimbo za Wigashe zimetafitiwa na kujadiliwa na wataalamu wengi kama Cory (1937, 1954), Stockley (1940), Chenya (1960), Masuha (1963), Ravindra (1971), Mkongola (1980), Kija (1987), Songoyi (1998), Lupande (1962, 1995), Nketia (1999), Gunderson (1999) na Makoye (1993, 1996, 2005, 2010). Uchunguzi wao umejikita katika aina moja ya wimbo wa kazi miongoni mwa nyimbo lukuki za kilimo pamoja na kazi nyinginezo, ilhali dhima ya nyimbo zote hushabihiana kulingana na shughuli inayofanyika. Nyimbo za kilimo ni jambo ambalo limeachwa nje ya utafiti kwa muda mrefu kwani tafiti hizi si za miaka ya karibuni wakati jamii inabadilika siku hadi siku. Jambo hili la dhima ya nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma bado ni suala linalohitaji utafiti wa hivi karibuni kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Stockley (1940) anaelezea kuwa manju huweza kutunga wimbo wa kusifia ardhi inayotoa mazao mengi yenye rutuba na kutilia mkazo ukulima wenye tija. Wasukuma walitambulisha ardhi kwa sifa zake. Kwa mfano, sehemu ya ardhi ngumu isiyo na rutuba nyingi na isiyootesha nyasi ndefu iliitwa bambasi; sehemu ya ardhi yenye udongo mwekundu ni ikulusi; sehemu ya ardhi ambayo haijalimwa kwa kipindi kirefu ni itogolo; sehemu ya ardhi yenye udongo wa kichanga ni jiseni/isanga; na sehemu ya ardhi ngumu yenye rutuba nyingi ni mbuga. Huu ni utafiti ulihusu matukio mbalimbali ya kiimani kuhusu ardhi wailimayo, maana Wasukuma pia hujikita sana katika masuala ya kiimani, yaani Mungu na miungu, ambapo huwa na nyimbo za kuitakasa ardhi kwa wakulima, wachimbaji na wafugaji pamoja na ziwa kwa wavuvi. Katika utafiti huu bado athari za nyimbo za kilimo zinahitaji mjadala.

Seif (2022) ametafiti kuhusu nyimbo za kiasili zinavyoimarisha mafunzo ya jadi nchini Tanzania kwa kujikita katika jamii ya Wakaguru mkoani Morogoro. Ameeleza kuwa nyimbo hizo zinasaidia kuifunza jamii masuala ya utamaduni, siasa na uchumi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Misingi ya mila, desturi, falsafa, historia na maendeleo yao inarejelewa katika vipengele vingi vya maisha ya jadi. Utafiti huu umesaidia kueleza mambo mbalimbali ya kitamaduni kwa kujikita katika nyimbo za matambiko, jando na unyago. Nyimbo za kazi, hususani za kilimo, hazijazungumziwa. Suala hili ndilo lengo la makala hii.

Wendo na mwenzake (2025) wametafiti juu ya maudhui ya ukungwi katika nyimbo za taarab na kusema kuwa kungwi ana jukumu la kuwafundisha wanawari kuhusu masuala ya unyumba, yakiwemo usafi wa mwili na nyumba, namna ya kumhudumia mume, namna ya kuzungumza na marafiki na jamaa wa mume, pamoja na matumizi ya vifaa vya kiasili kama vile mbuzi, kinu, mchi na ufagio miongoni mwa mengine. Maudhui haya ya ukungwi hufundishwa na waimbaji wa nyimbo teule za taarab. Utafiti huu umekuwa muhimu katika kueleza aina mbalimbali za nyimbo pamoja na maudhui yake yanayowasilishwa, ingawa haujagusia nyimbo za kilimo. Kwa hiyo, nyimbo katika makabila mbalimbali hutoa mafunzo kadha wa kadha katika jamii, na hata maudhui yake huweza kutofautiana kulingana na matakwa ya jamii husika. Hata suala la dhima huweza kutofautiana baina ya jamii moja na nyingine. Hii hutokana na kwamba shughuli nyingi za jamii huegemezwa katika misingi imara ya mila na desturi zao katika uendeshaji wake kutoka kizazi hadi kizazi. Mpaka sasa zipo jamii nyingi nchini Tanzania zenye viashiria vya kufuata mila na desturi zake kwa kuzingatia mabadiliko ya wakati. Makala hii imeshughulikia athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma katika jamii ya leo.

## 3.0 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu umefanyika mkoani Mwanza, wilaya ya Kwimba, katika kijiji cha Mbulya, kata ya Ngula. Data za utafiti huu zimekusanywa kutoka eneo tajwa, japo zingeweza kukusanywa kutoka eneo lolote katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Simiyu, maana shughuli zifanywazo na Wasukuma wa mikoa hiyo zinafanana na tamaduni zao zinashabihiana kwa ukaribu. Lengo la kuteua eneo hilo ni sababu za kiuchumi kulingana na uzoefu na uenyeji wa mtafiti, maana wilaya ya Kwimba ndiko aliweza kufika na kukusanya data kwa urahisi kuliko sehemu nyinginezo. Eneo hilo limechaguliwa kimakusudi kuwakilisha mikoa mingine na wilaya zake wanamoishi Wasukuma.

Utafiti umetumia data za aina mbili: za msingi na za upili. Data za msingi zilipatikana kwa kutumia mbinu za mahojiano na ushuhudiaji, ambapo mahojiano yalihusisha wazee wanaofundisha mambo mbalimbali ya kitamaduni zikiwemo nyimbo, maigizo na mavazi; vijana wanaolima kwa umoja; wake kwa waume; pamoja na viongozi wa vikundi vya kijamii katika vijiji (koo). Wazee ndio wanaojua mila na desturi, yakiwemo mafundisho ya rika kwa rika pamoja na nyimbo za aina mbalimbali, hasa za kilimo.

Wazee ndio hufundisha nyimbo za kilimo za kipindi cha kulima, kupanda, kuvuna na kufanya sherehe za mavuno ambazo huwa kama mashindano ya koo kwa koo katika kuonesha walivyovuna na namna wanavyotumbuiza wakati wa kuonesha mavuno yao. Rika zote huhusishwa katika nyimbo za sherehe za mavuno, lakini katika kuandaa mashamba, kulima na kuvuna huhusishwa watu wazima wanaoweza kufanya kazi kwa bidii, huku vijana wadogo wakiendelea na shughuli zao za uchungaji wa mifugo na uvuvi wa samaki. Mbinu ya ushuhudiaji imetumika katika kukusanya nyimbo za kilimo katika hatua zote kuanzia kuandaa mashamba, kupanda, kuvuna na kufanya sherehe za mavuno.

Data za upili zimekusanywa kwa kupitia nyaraka za maktabani kuhusu jamii za Wasukuma na shughuli zao za kijamii na kiuchumi. Vilevile, zimepitiwa nyaraka kuhusu tafiti mbalimbali za fasihi simulizi kuhusu nyimbo zinazohusu tamaduni mbalimbali za Kiafrika, hususani Wasukuma katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Nyaraka zote hizi zimesaidia kujenga uelewa juu ya mada ya utafiti kuhusu athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma. Hata hivyo, katika upitiaji wa nyaraka imebainika kuwa nyimbo zimetafitiwa kwa upana wake katika jamii za Wakerewe, Wanyamwezi, Wajita na Wahaya (Kezilahabi, 1981), ingawa nyimbo za kilimo za Wasukuma zimetajwa kijumla kuwa zipo na zinafanywa, ila hazijatafitiwa kwa kina. Nyaraka hizi zimekuwa msaada katika kupata maarifa ya nyimbo kwa ujumla na kutoa mwanga wa kukiendea kile ambacho ni lengo la utafiti huu.

Maktaba zilizotumika ni za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hasa sehemu ya East Africana ambako kuna tafiti mbalimbali; Maktaba Kuu ya Taifa; Maktaba ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Mwanza; pamoja

na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Bishop Stuart, Mbarara, Uganda. Maktaba hizi zimejaa nyaraka mbalimbali zilizotoa data zilizokuwa zinahitajika katika kukamilisha utafiti huu.

### 3.1Nadharia Zilizotumika Katika Makala Haya

#### 3.1.1Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi

Nadharia hii muasisi wake ni (Georg Lukacs 1885–1971), ambapo anaeleza kuwa nadharia ya sosholojia ya fasihi inalenga kuchunguza mahusiano kati ya sanaa, umma na muundo wa kijamii. Lengo la nadharia hii ni kufafanua sababu zinazopelekea kuzuka kwa kazi ya sanaa inayofumbata masuala ya jamii na jinsi ambavyo ubunifu wa mwanafasihi unavyomwongoza katika kuzieleza mila, desturi na mipangilio ya jamii husika (Coser, 1963).

Nadharia hii inaonesha kuwa kazi za fasihi huakisi mila na desturi pamoja na masuala mbalimbali ya kijamii. Mazingira ya kijamii ndiyo huipelekea kazi ya fasihi iwe katika umbo fulani. Kazi ya kifasihi huiakisi jamii lengwa. Kwa vile kazi ya fasihi ni zao la jamii, huwasilisha yale iyaonayo ndani ya jamii. Haya yanaelezwa na Kenyance (2018) pamoja na Njogu na Chimerah (1999) wanaposisitiza kuwa fasihi inaangalia maisha ya jamii halisi na kuwakilisha yale yaliyomo katika jamii hiyo. Wanasisitiza kuwa sosholojia ya fasihi humzingatia binadamu kama uti wa mgongo wa ulimwengu na sanaa yake. Mtunzi wa kazi ya fasihi hawezi kukwepa athari za kijamii katika kazi yake, maana kazi hiyo ni muakisi wa kile kilichomo katika jamii husika.

Nadharia ya sosholojia katika makala hii imetoa mwongozo katika kuzikusanya nyimbo za kilimo katika hatua mbalimbali za kuandaa mashamba, kulima, kupanda na kuvuna pamoja na nyimbo za sherehe za mavuno. Nyimbo hizi za kilimo zimeakisi mila, desturi na nguvu ya sanaa katika utendaji kazi miongoni mwa jamii za Wasukuma. Nadharia pia imesaidia katika kuzichambua nyimbo hizo ambazo zimekuwa kielelezo cha utamaduni wa Wasukuma katika kazi zao za kilimo na jinsi ambavyo nyimbo hizo huleta athari mbalimbali kulingana na maudhui yanayowasilishwa katika nyimbo hizo za kilimo.

#### 3.1.2 Nadharia ya Utendaji wa Maigizo

Waasisi wa nadharia ya utendaji wa maigizo ni kama vile (Bauman, 1975), (Foley, 1995) na (Schechner, 2013), ambao wanashikilia kuwa wahakiki sharti wachunguze zaidi ya matini moja na kuhakiki utendaji unaoambatana na matini husika. Mihimili ya nadharia iliyotumiwa ni ifuatayo:

(i)Muundo wa tukio la kiutendaji kulingana na muktadha wa uwasilishaji.
(ii)Utangamano wa fanani na hadhira wakati wa uwasilishaji wa fasihi.
(iii)Mfanyiko wa kimawasiliano kulingana na kaida za utamaduni wa jamii inayochunguzwa.

Kwa mujibu wa (Schechner, 2013), utendaji ni tukio la aina yoyote linalowajumuisha hadhira pamoja na fanani wake kwa minajili ya kuigiza au kuonesha tabia za wanadamu. Kutokana na maelezo yake, mipaka kati ya utendaji unaotokea katika kazi za kisanaa kwa upande mmoja na utendaji unaotokea katika shughuli za kila siku kwa upande mwingine ni wa kidhahania.

Kwa mujibu wa (Brunolt, 2013) pamoja na (Mulokozi, 2002), uhakiki wa fasihi simulizi ya Kiafrika unapaswa kuzingatia namna fasihi hiyo inavyotendwa kwa kuwasilishwa mbele ya hadhira. Kwa ufupi, Mulokozi anaonelea kuwa msingi mkuu wa nadharia ya utendaji ni muktadha unaojumuisha fanani, hadhira, tukio na lugha. Kwa upande mwingine, Alembi na Mulokozi wanatoa mawazo kuwa utendaji ni uti wa mgongo wa fasihi simulizi. Ndani ya utendaji huo, fanani huanzisha mawasiliano na hadhira hushiriki moja kwa moja katika kukamilisha mawasiliano kwa njia ya kuuliza, kuelekeza, kuimba na kujibu maswali ya fanani. Kadhalika, fanani anaweza kuupa nguvu utendaji wake kwa kutumia si tu lugha ya maneno ya mdomo, bali pia mitindo ya viziada lugha kama vile ishara za uso, mikono, kichwa na sauti wakati wa kuwasilisha sanaa yake.

Kwa upande wake, (Okpewho, 1992) anaona kuwa utendaji wa fasihi simulizi ya Kiafrika unapaswa kuzingatia si tu maneno yanayotamkwa kwa kutumia lugha ya mdomo, bali pia ujumbe unaowasilishwa kwa kutumia lugha ya ishara au viziada lugha. Hii ni mbinu ya mawasiliano inayotumia ishara za uso, mikono, uchezaji pamoja na sauti, hususan sauti za kimuziki. Mtaalamu huyu anasisitiza kuwa, mbali na maneno ya mdomo, wasanii wa fasihi simulizi hutumia mbinu mbadala katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

Katika kuchunguza utendaji wa nyimbo za kilimo, mawazo ya Okpewho yametumika kwa kiwango kikubwa. Mawazo haya yametumika katika kuchanganua

mikakati ya utendaji unaofanywa kwa kutumia lugha, muziki na uigizaji ndani ya nyimbo hizo. Hii ni kwa sababu uwasilishaji wa nyimbo za kilimo unahusisha matumizi ya sauti na mapigo ya kimuziki kwa njia ya uimbaji na matumizi ya ala za muziki. Matumizi ya mbinu za uchezaji na uigizaji pia yamechunguzwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya utendaji iliyopendekezwa na Okpewho.

## 4.0 MATOKEO YA UTAFITI

### 4.1 Ubainishaji wa Nyimbo za Kilimo katika Jamii ya Wasukuma

Lengo la kwanza la utafiti lilikuwa kubainisha nyimbo za kilimo zinazotumiwa katika jamii ya Wasukuma. Kila jamii huwa na nyimbo zake, na thamani ya nyimbo inadhihirishwa na jamii husika kwa kuzipa nafasi yake kulingana na tukio (Rajwayi, 2009).

Hivyo, kwa msaada wa watafitiwa, utafiti umeweza kubaini nyimbo mbalimbali zinazotumiwa na wanajamii hawa katika shughuli nzima ya kilimo, ikiwemo nyimbo za wakati wa kupanda, kupalilia na kuvuna. Nyimbo hizo ni kama zifuatazo:

**1. Wimbo wa Kupanda Mchele**

**Maneno ya Nyimbo**

Nalime mchele Zoleka,
nalime mchele na lyongo lumala nduhu ukutabuka aa
Wote: /inzala mbuli itatulaga hodi hangi iti na ntale

**Fasiri ya Kiswahili**

Nilime mpunga Zoleka, nilime mpunga na mhogo, hakuna kutaabika.
Wote: Njaa mjinga habishi hodi tena hana mkubwa.

**2. Wimbo wa Kupalilia**

Maneno ya Nyimbo:
Ndhi sata mhunda ×2, Katalina natukwibaga.
Onilisha makhi onilisha makhi Katalina natukwibagaaa
Wote: tinginaga egiseli ili chuma lyane ×2 lyanilililanigandya

**Fasiri ya Kiswahili**

Naumwa tumbo ×2, Katalina sikusahau umenilisha nini,
Umenilisha nini Katalina sikusahau.
Kiitikio / tikisika ekseli chuma langu ×2, hili litanikondesha.

**3. Wimbo wa Palizi**

**Maneno ya Nyimbo**

Ghudimagi umphini mugudame,
ihakiba yaya ukwibhi bhasumba,
ubhebhe uluugayiwa ng'ombe,
abhana bako ulabhayanjaaaa.
Ulu ulachaga ubhebhe baduguyo,
bandya kubuja ya numa,
ubhise tulibuja kachile,
ka ng'wamarehemu akaleka mhayo kiii.
Abhana bako bandya kuhaya,
Ayombe makhi isabho wapembaaaa

**Fasiri ya Kiswahili**

Shikeni mpini imara,
Akiba msisahau vijana,
Wewe ukikosa ng'ombe,
Watoto wako watakuwa wanachanganyikiwa.
Siku ukifa ndugu zako,
Wataanza kuuliza ya nyuma,
Sisi tunauliza mauti ya marehemu,
Aliacha neno gani?
Watoto wako wataanza kusema,
Aseme nini mali amemaliza.

**4. Wimbo wa Mavuno**

**Maneno ya Nyimbo**

Magisi ulu nulima buluba,
natajingaga abhakima ×2
Wote: nibuli abhoyi batatubujaga

**Fasiri ya Kiswahili**

Maksi nikilima pamba,
Sitongozi wanawake ×2
Wote: Kwanini wao hawatuulizi?

**Maneno ya Nyimbo**

Ikungulume lyahila,
Mami mami mishaga wela,
Wela bho milimo hangi ×2

**Fasiri ya Kiswahili**

Jogoo limewika,
Mjomba mjomba amka, kumekucha,
Kumekucha, tufanye kazi tena ×2

### 4.2 Dhima za Nyimbo katika Jamii ya Wasukuma

Dhima ni wajibu mkubwa pamoja na uwezo wa kufanya jambo. Katika kukidhi lengo la pili la utafiti huu, ambalo lilikuwa kueleza dhima za nyimbo katika jamii ya

Wasukuma na kubaini na kuchunguza athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma, watoa taarifa thelathini na tisa, ambao ni sawa na asilimia tisini na nane ya watoa taarifa wote, walionyesha kufanana kwa majibu yao. Na mtafitiwa mmoja tu aliongeza hoja ambayo ilikuwa tofauti na watoa taarifa wengine katika kueleza dhima za nyimbo katika jamii yao ya Wasukuma, ambayo ni sawa na asilimia mbili. Kulingana na idadi kubwa ya watoa taarifa kushabihiana kwa majibu yao na kuthibitisha kuwepo kwa athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma, watafiti walikubaliana na athari hizo. Kwa hiyo, utafiti umebaini dhima zifuatazo:

#### 4.2.1 Dhima ya Kuhamasisha Watu katika Shughuli Mbalimbali

Nyimbo hizi za kilimo katika jamii ya Wasukuma zina lengo la kuhamasisha jamii ili kujishughulisha katika kazi za kilimo, hasa kilimo cha mpunga na muhogo, ili kujinasua na janga la njaa, kama inavyojionyesha katika wimbo ufuatao:

**Maneno ya Nyimbo**

Nalime mchele Zoleka,
Nalime mchele na lyongo lumala nduhu ukutabuka aa
Wote: /inzala mbuli itatulaga hodi hangi iti na ntale

Hivyo, wimbo huu unahamasisha watu kufanya kazi za kilimo ili kujikinga na njaa ambayo haichagui mkubwa wala mdogo. Jambo hili linaelezwa na (Mlama, 1983) anaposisitiza masuala ya utendaji kuwa ni jambo la msingi katika kuhamasisha jamii katika kazi mbalimbali za kiutendaji. Kilimo ni kazi mojawapo ya kiutendaji inayohusiana na nyimbo.

#### 4.2.2 Dhima ya Kuonesha Hisia Zilizo Ndani ya Mtu au Watu

Dhima hii ilielezwa na mtafitiwa mmoja, ambaye ni sawa na asilimia mbili ya watoa taarifa. Japo ni idadi ndogo, mtafiti alikubaliana na hoja hii kama nyongeza ya hoja nyingine zilizopatikana kutoka kwa watoa taarifa wengine. Utafiti unaonyesha kwamba nyimbo hizi za kilimo hazizungumzii masuala ya kilimo tu, bali pia hutoa nafasi ya kuonesha hisia za watu. Katika wimbo ufuatao, mwimbaji anaonesha hisia ya mapenzi kwa kuonyesha upendo aliokuwa nao kwa mkewe (Katalina). Mwimbaji analalamika kuwa anashindwa kumsahau, ni nini alichomlisha, hata kila mara anamkumbuka. Hivyo basi, mwimbaji ameweza kuonesha hisia zake za ndani kwa kueleza jamii kwa njia ya wimbo:

**Maneno ya Nyimbo**

Ndhi sata mhunda ×2, Katalina natukwibaga
Onilisha makhi onilisha makhi Katalina natukwibagaaa
Wote: tinginaga egiseli ili chuma lyane ×2 lyanilililanigandya

Katika mazingira ya kazi katika jamii ya Wasukuma, mchapakazi hupata mchumba mapema kutokana na ukubalifu katika jamii. Ndio maana nyimbo za hisia za mapenzi hutumiwa sana katika kilimo, ikiwa na maana ya kuwa wawe wachapakazi ili wapate wachumba. Masuala haya ya kitamaduni yanaungwa mkono na (Masinjila, 1994) katika kuhamasisha ufundishwaji wa fasihi simulizi katika jamii.

#### 4.2.3 Dhima ya Kuburudisha Wakulima na Kuchochea Utendaji

Watafitiwa 38, ambao ni sawa na asilimia tisini na tano, walionekana kufanana katika hoja hii, jambo ambalo liliwashawishi watoa taarifa wengine kuikubali. Wakulima wa jamii ya Wasukuma walidai kuwa wanapolima kwa kuimba wanaburudika na kupata nguvu ya kulima eneo kubwa bila kuchoka na kwa haraka, hata kutoka alfajiri hadi machweo. Hivyo, wanapolima kwa kufuata mapigo ya muziki, huweza kufanya kazi muda mrefu bila uchovu. Hii ni kwa sababu nyimbo tofauti zenye mapigo tofauti ya kimuziki huimbwa sambamba na kazi.

Hoja hii imefafanuliwa vizuri na (Makoye, 2005) kuhusu burudani zinazopatikana katika nyimbo za asili. Anafafanua kuwa nyimbo za asili zinakuwa na mguso wa tofauti ukilinganisha na nyimbo za kigeni, ambazo wazawa wengi huimba bila kutilia maanani ujumbe uliomo.

#### 4.2.4 Dhima ya Kufundisha Maadili

Kiasi kikubwa cha watoa taarifa, sawa na asilimia tisini na sita, walionyesha kuwepo kwa dhima hii, ambayo inatokana na nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma. Maadili yalifundishwa kwa kuzingatia umri na nafasi au wajibu katika jamii. Katika wimbo ufuatao, unaonyesha jinsi wanavyofundisha vijana kuwa na juhudi ya kufanya kazi na umuhimu wa kuweka akiba kwa matumizi ya baadaye:

**Maneno ya Nyimbo**

Ghudimagi umphini mugudame,
Ihakiba yaya ukwibhi bhasumba,
Ubhebhe uluugayiwa ng’ombe,

Abhana bako ulabhayanjaaaa.
Ulu ulachaga ubhebhe baduguyo,
Bandya kubuja ya numa,
Ubhise tulibuja kachile,
Ka ng'wamarehemu akaleka mhayo kiii.
Abhana bako bandya kuhaya,
Ayombe makhi isabho wapembaaaa

Kila jamii inakuwa na utamaduni wake. Jamii ya Wasukuma inathamini sana mifugo kama sehemu ya urithi. Kila baba wa kaya na familia yake ni muhimu kutunza tamaduni hizo ili watoto wake waendelee kuziendeleza. Nyimbo za kilimo na za harusi husisitiza haya kama anavyoeleza (Yonazi, 2019).

#### 4.2.5 Dhima ya Kutambulisha Utamaduni wa Jamii Husika

Kwa mujibu wa watoa taarifa thelathini na tisa, sawa na asilimia tisini na nane, walionesha kuwepo kwa dhima ya kutambulisha utamaduni katika nyimbo za kilimo. Katika jamii ya Wasukuma, nyimbo huimbwa ili kuonyesha utamaduni wao. Wimbo uliooneshwa hapa chini unaonyesha utamaduni wa Wasukuma katika mahusiano (ndoa) wakati wa mavuno. Wimbo unaonesha jinsi wanaume wanapokuwa na pesa baada ya mavuno, huwa wanatafuta wanawake kwa ajili ya mahusiano ya kimahusiano. Fanani wa wimbo anaonyesha dalili zote za kupinga kitendo hicho na kuonyesha hasira dhidi ya wanaume wenye tabia ya kufuja mali kwa kustarehe na wanawake baada ya mavuno, jambo linaloathiri maendeleo.

**Maneno ya Nyimbo**

Magisi ulu nulima buluba,
Natajingaga abhakima ×2
Wote: nibuli abhoyi batatubujaga

Wanaume katika jamii nyingi za Kiafrika wnapokuwa na pesa huwaza kuongeza wake au mahusiano ya mapenzi. Jambo hili hujidhihirisha katika nyimbo nyingi za kitamaduni za kazi na za harusi. Inaelezwa na (Waziri, 2016) katika nyimbo za harusi Zanzibar.

#### 4.2.6 Dhima ya Kukuza Talanta na Sanaa

Malcolm (1993) anaeleza kuwa Wasukuma hawakuchagua kazi; kwao kazi ngumu waliiona rahisi. Kutokana na kufanya kazi hizo ngumu, walipendelea sana kuimba nyimbo kulingana na tukio. Nyimbo zilichukuliwa kama sehemu ya utambulisho wa Wasukuma popote alipokuwa. Makoye (2005) anasema kuwa nyimbo ni roho ya utamaduni wa Wasukuma popote inapoimbwa. Sababu nyingine ya kupenda nyimbo hizi ni ushindani baina ya kundi moja na lingine na matumizi ya sihiri za kiwango cha juu, ambazo zilikuwa na uwezo wa kuwadhohofisha wapinzani na kuongeza wafuasi wa kundi husika.

Asilimia themanini na nane ya watoa taarifa wote walieleza kwamba nyimbo za kilimo zinaweza kutumika kama njia ya kukuza talanta na sanaa. Hii inatokana na ukweli kwamba jamii ya Wasukuma si wote wenye kipaji cha kuimba; wale wanaoweza na wanaopenda kuimba ndiyo njia pekee ya kukuza talanta hiyo. Pia, uwezo wa kubuni na kutunga nyimbo unakuzwa sana, hasa pale jamii inapokuwa tayari kuziimba nyimbo hizo katika shughuli mbalimbali za kilimo, kuanzia kupanda, kupalilia hadi kuvuna.

### 4.3 Kukuza Ushirikiano na Umoja Katika Kazi

Watafitiwa arobaini, sawa na asilimia mia moja, walieleza kuwa nyimbo za kilimo zina dhima ya kukuza ushirikiano na umoja katika kazi katika jamii yao. Wasukuma wa wilaya ya Kwimba hutumia nyimbo wakati wa kilimo kama nyenzo ya kudumisha ushirikiano na umoja. Nyimbo ndizo zinazowaunganisha pamoja; wanaimba pamoja na kushiriki matendo yote yanayohusiana na nyimbo, kisha wanakula na kunywa pamoja. Hali hii inafanya watu wafahamiane na kukuza uhusiano na ushirikiano miongoni mwao, hivyo kurahisisha kazi. Jambo hili limeelezwa na (Omari, 2009) katika utafiti wake kuhusu nyimbo za Hip Hop, ambapo anaeleza kuwa ushirikiano ni nyenzo ya maendeleo.

Kutokana na ujumbe na malengo ya nyimbo hizi, ni wazi kuwa nyimbo zinakubaliana moja kwa moja na nadharia ya uamilifu, inayodai kwamba kazi yoyote ya fasihi lazima iwe na lengo fulani au ilenge kuleta ujumbe fulani katika jamii. Ndivyo utafiti ulivyoonyesha kuwa kila wimbo ulioimbwa ulikuwa na lengo fulani, aidha la kuburudisha, kuonyesha hisia, au kuleta umoja na ushirikiano miongoni mwa wanajamii.

### 4.4 Mapendekezo ya Kudumisha Nyimbo za Kilimo za Kisukuma

Lengo la tatu lilikuwa kutoa mapendekezo kuhusu jinsi ya kudumisha nyimbo hizo za Wasukuma. Kupitia mahojiano na watoa taarifa, watafiti waliweza kupata mapendekezo yafuatayo:

1. Kuhifadhi nyimbo za jamii ya Wasukuma katika machapisho mbalimbali ili ziweze kutumika na vizazi vijavyo. Pia kuzihifadhi kwenye kanda ili vizazi vijavyo viweze kujua namna ya kuziimba nyimbo hizo.

2. Kuhamasisha watu wote wa jamii ya Wasukuma kuthamini nyimbo hizo, kwani ni kitambulisho cha jamii yao au utamaduni wao. Wasukuma, hasa vijana, wahamasishwe kuthamini nyimbo za utamaduni kuliko nyimbo za kizazi kipya. Watambue nafasi ya nyimbo hizi za kilimo katika kuendeleza uzalishaji mali, na hivyo nyimbo hizi zinaweza kuendelezwa katika jamii hii.
3. Kuanzisha siku maalumu ya maadhimisho ya nyimbo hizo miongoni mwa jamii hii ya Wasukuma. Siku hiyo itumike kutoa mawazo na kuhamasisha utungaji wa nyimbo mpya, watu watazisikia nyimbo hizo, na hivyo kusaidia kueneza na kuhifadhi nyimbo hizo.

4. Kuweka nyimbo hizo katika mtandao ili watoto au kizazi cha sasa kuzijue. Hii itarahisisha elimu na maarifa, kwani kizazi cha sasa hupata elimu kutoka kwenye mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter na Instagram.

5. Kukusanya nyimbo zote na kuziweka katika maandishi ili kupunguza kupotea na kusahau kwa nyimbo hizo. Hii ni muhimu kwani nyimbo nyingi zipo vichwani mwa watu wazima, hususan wazee wa zamani, na ni rahisi kupotea. Juhudi kubwa lazima zifanyike katika kuhifadhi nyimbo hizi katika mifumo ya kisasa kama vile kompyuta, tepu, rekoda na CD.

### 5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Nyimbo za kilimo katika jamii za Wasukuma zimebeba maudhui mbalimbali ambayo yanaifanya jamii iendelee kuuthamini ukale bila kuuathiri usasa katika maisha yao. Nyimbo hizo zina athari mbalimbali kwa wanajamii, kama ilivyoainishwa katika nyimbo mahususi. Hata hivyo, jamii inakuwa na baadhi ya watu ambao ni wavivu, wenye ukosefu wa uzalendo, upendo, na ushirikiano. Hii ni kutokana na kukosekana kwa malezi bora kwa baadhi ya familia kwa vijana wao na kupelekea wao kupuuza mila na desturi kwa kudhani ni mambo ya kale. Jamii inapofanya kazi kwa umoja, huwa chachu ya mabadiliko na kuifanya jamii kuwa na maendeleo kutokana na matunda ya kazi wanazozifanya wanajamii.

Tumekuwa na jamii ya vijana wasiopenda kazi, ambao wanapendelea kubeti, kuangalia runinga wakati wa kazi, kuolewa au kuoa watu wazima wanaoamini watawakuta kila kitu bila kuangalia juhudi za kufanya kazi ngumu kama kilimo ili kujitafutia mahitaji ya kila siku. Haya yote ni matunda ya vijana kuuacha ukale na kudhani ni wa kisasa zaidi. Jamii haiwezi kushikilia ukale tu na kuuacha usasa, bali ni vyema kuchaganya vyote kwa pamoja ili kuunda jamii ya sasa yenye kuushikilia ukale wenye manufaa endelevu, kama vile hamasa ya kazi na kuleta umoja wa jamii pamoja.

Nadharia ya usosholojia ya fasihi imewezesha makala hii kukamilika kwa kuonesha jinsi nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma zinavyowaleta watu pamoja na kuwafanya waishi kwa kufanya kazi kwa umoja. Nadharia imeonyesha jinsi nyimbo za kilimo zinavyojamiisha jamii na kuwafanya wanajamii kutenda kwa mshikamano. Hata hivyo, nadharia ya utendaji wa maigizo, kupitia mihimili yake, tumeona jinsi nyimbo za kilimo za Wasukuma zinavyowahamasisha wakulima katika utendaji wa aina mbalimbali. Wanapokuwa wanalima, kama alivyoeleza (Okpewho, 1992), utendaji hauhusishi sauti tu za kuimba, bali pia vitendo mbalimbali kama kuigiza, kuruka, kutingisha mikono, kupiga makofi, kushangilia kwa kutumia viungo vya mwili, na matendo mengineyo.

Kipindi cha mavuno kinaambatana na sherehe mbalimbali ili kukuza ushindani baina ya jamii zao. Hii husaidia kukuza ubunifu kwa kuambatana na maleba, ngoma za kucheza aina mbalimbali, na kula na kunywa pamoja. Huwa kuna mapishi mbalimbali wakati wa kuonesha baadhi ya mazao waliyoyavuna. Makala hii pia imeshughulikia nguvu za kijamii na nguvu za kisanaa miongoni mwa jamii za Wasukuma. Baadhi ya koo huleta sanaa za hali ya juu kama vile mazingaombwe ya kucheza na nyoka, kumeza moto na kuutema, kurusha vitu vya hatari kama mkuki na kuvidaka bila kuwadhuru, na mengineyo yanayofanana na hayo. Utendaji wa namna hii unakuza ubunifu katika nyanja hizo, maana matendo hayo huambatana na nyimbo.

Uwanda wa nyimbo kama sehemu ya fasihi simulizi ni mpana sana, na ndio maana makala hii imejikita katika kuchunguza nyimbo za kilimo za Wasukuma, kwani watafiti wengi wametafiti nyimbo nyingine na za kilimo

kubakia nyuma. Nyimbo hizi zimekuwa zikitajwa tu na watafiti kama vile (Masanja, 2019).

Kazi ya fasihi inadhibitiwa na mifumo iliyopo katika jamii katika kuihifadhi kwa njia ya utendaji na nyimbo kama ilivyobainishwa. Uhusiano uliopo katika jamii na mienendo yake husaidia jamii kuwa pamoja na kuendelea kufanya utendaji mbalimbali unaoiweka jamii pamoja. Nyimbo za kilimo zinatazamwa kama kielelezo cha ukuaji wa uchumi, siasa, mila, na desturi, na kuipelekea jamii kubadilika hatua kwa hatua kadri inavyofanya shughuli mbalimbali, ikiwemo kilimo kinachoiweka jamii pamoja. Nadharia ya usosholojia wa fasihi na utendaji wa maigizo zimemwezesha mtafiti kuzichunguza athari za nyimbo za kilimo katika jamii ya Wasukuma, ambazo huleta jamii pamoja kwa kuhusisha utendaji mbalimbali katika kazi zao za kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara.

**Mapendekezo: Mapendekezo kwa Wanataaluma**

Watafiti wanashauri watafiti na wanataaluma kuthamini lugha ya Kiswahili na lugha zetu za Kibantu kwa kufanya tafiti mbalimbali, hasa katika uwanja wa fasihi simulizi, badala ya kufanya tafiti kwa lugha ya Kiingereza. Hii itasaidia kukuza na kuhifadhi tamaduni zetu.

Pia, tunapendekeza wizara ya michezo na utamaduni ipe ufadhili kwa watu wanaotaka kutoa machapisho ya tafiti zao, hasa zilizofanywa kwa lugha ya Kiswahili au Kibantu,
ili kuzihifadhi kwa vizazi vijavyo.

**Mapendekezo kwa Watafiti Wajao**

Kutokana na utafiti huu kuzingatia muda mdogo, haukufanikisha kutafiti aina zote za nyimbo. Kwa hiyo, watafiti wanapendekeza kuwa watafiti wa baadaye wachunguze aina nyingine za nyimbo, kama vile nyimbo za tukuzo, nyimbo za tumbuizo, na nyimbo za tendi au tenzi zinazotumika katika jamii ya Wasukuma. Hii itasaidia kukusanya nyimbo nyingi na kuziweka katika maandishi.

## 6.0 MAREJELEO


Asajile, R. S. (2020). Maadili katika nyimbo za harusi za jamii ya Wanyakyusa. *EANSO, 8*(1), 144–155. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.2688

Bauman, R. (1975). Verbal arts as performance. *American Anthropologist, New Series, 77*(2), 290–311. https://doi.org/10.1525/aa.1975.77.2.02a00030

Budebah, B. C., & Bakize, H. L. (2014). Mbinu za utunzi wa nyimbo ndefu katika ngoma za Wigashe. *UDSM Administrator+Journal+Manager, 7*(3), 87–99. https://journals.udsm.ac.tz/index.php/kcl/article/view/992/922

Finnegan, R. (1970). *Oral literature in Africa*. Cambridge: Open Book Publishers. https://www.openbookpublishers.com/books/10.11647/obp.0025

Finnegan, R. (1983). *Oral literature in Africa*. Oxford University Press. https://library.oapen.org/bitstream/id/6fde2200-2c9e-48cc-8fc7-d556ee6a90b3/633751.pdf

Finnegan, R. (1992). *Oral traditions and the verbal arts: A guide to research practices*. https://doi.org/10.4324/9780203393215

Finnegan, R. (2015). *Where is language?* London: Bloomsbury. https://doi.org/10.1017/S0047404518000118

Foley, J. (1995). *The singer of the tales: Performance*. Bloomington, IN: Indiana University Press. https://www.academia.edu/120077577/John_Miles_Foley_The_Singer_of_Tales_in_Performance

Josphat, M. E., et al. (2022). Maudhui katika nyimbo za Tohara zilizodenguliwa na nyimbo za Dini za Kiigembe katika kuafikia maendeleo endelevu kwa Waigembe. *EANSO, 5*(1), 273–287. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.813

Kadallah, T. R. (2018). Utendaji katika nyimbo za ngomaya Wasambaa: Mifano kutoka Mdumange nchini Tanzania (Master's thesis, Moi University, unpublished).

Kezilahabi, E. (1981). Ushairi na nyimbo katika utamaduni. In *Urithi wa Utamaduni Wetu*. Tanzania Publishing House. https://ul.qucosa.de/api/qucosa%3A72133/attachment/ATT-0/

Kiango, S. D. (1992). Taswira ya mwanamke katika tamthiliya za Kiswahili za Kenya. *Jarida la Kiswahili, Baragumu, 1*(2), 32–58. https://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/11537

King'ei, K., & Ndalu, A. (2009). *Kamusi ya Mithali* (Toleo jipya). Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Kuvuna, N. M. (2013). Mtindo katika nyimbo za kazi za jamii ya Warabai (Master's thesis, Kenyatta University, unpublished).

Lukacs, G. (1962). *Preface to the theory of the novel*. Franklin: Merlin Press. https://www.marxists.org/archive/lukacs/works/theory-novel/preface.htm

Makoye, H. (1996). Tanzania traditional dances, choreography and communication in urban Dar es Salaam (M.A. thesis, University of Dar es Salaam). https://phaidra.univie.ac.at/api/object/o:1259495/download

Makoye, H. (2005). Training and natural endowment in Sukuma dance culture. *UTAFITI Journal, 6*(2).

Makoye, H. (2010). *Studies in Sukuma dance culture*. Moshi: Shule & Co. Ltd.

Malcolm, W. (1953). *Sukumaland: An African people and their country*. London: Oxford University Press. https://www.africabib.org/rec.php?RID=268478775

Masanja, T. N. (2019). Uchunguzi wa kisemantiki wa majina ya asili katika koo za Ginantuzu (Master's thesis, Open University of Tanzania, unpublished).

Masinjila, M. (1994). *Teaching oral literature*. Kenya Oral Literature Association. https://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/51491

Mbijima, J. R. (2023). Nyimbo za jando za jamii ya Wagogo na maudhui yake. *Kioo cha Lugha, 21*(1), 160–182. https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.10

Miruko, R. S. H. (2016). Kuchunguza dhima za nyimbo za ngoma ya Kibati mkowa wa Kusini Pemba (Master's thesis, Open University of Tanzania, unpublished).

Mlama, P. M. (1983). A Tanzanian traditional theatre as pedagogical institution: The Kaguru theatre as a case study (Master's thesis, University of Dar es Salaam, unpublished).

Mulokozi, M. M. (2002). *The African epic controversy: Historical, philosophical and aesthetic perspectives on poetry and performance*. Mkuki na Nyota.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi simulizi na andishi*. Dar es Salaam: Moccony Limited.

Mwangosi, G. (2017). Usawiri wa nyimbo za magosi za Wanyakyusa katika muktadha wa Tanzania. *RUJASS, 3*, 92–124. https://iris.unito.it/retrieve/e27ce42c-76b4-2581-e053-d805fe0acbaa/swahili-Urban_Literature_2017.pdf

Ng'ata, G. J. (2023). Uchanganuzi wa nyimbo za Jaguar (Charles Njagua Kanyi) na Willy Paul (Wilson Abubakar Radido) (Master's thesis, Kenyatta University, unpublished).

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation. https://books.google.com/books/about/Ufundishaji_wa_fasihi.html?id=z4RkAAAAMAAJ

Okpewho, I. (1992). *African oral literature: Backgrounds, character, and continuity*. Indiana University Press. https://books.google.com/books/about/African_Oral_Literature.html?id=Az0O28OtWh4C

Omari, S. (2009). Hip hop music as popular oral poetry (Master's thesis, University of Dar es Salaam, unpublished).

Rajwayi, C. A. (2009). Maudhui na mtindo katika nyimbo za msanii Faustin Munishi (Master's thesis, Kenyatta University, unpublished).

Ravindra, D. (1971). *Studies of farm economics in Sukumaland and West Lake Region*. Tanzania: Ministry of Agriculture & Co-operative. https://edepot.wur.nl/136410

Schechner, R. (2013). *Performance studies: An introduction*. New York: Routledge.

Seif, D. G. (2023). Nyimbo za asili zinavyoimarisha mafunzo ya jadi nchini Tanzania. *RUJASS, 1*(1), 34–53. https://rucu.ac.tz/journals/articles/article-file/B46A7FD0.pdf

Simiyu, W. F. (2007). Nyiso za Wabukusu: Maudhui na lugha (Master's thesis, Kenyatta University, unpublished).

Simiyu, W. F. (2015). Mwingilianotanzu katika fasihi simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa (Master's thesis, Kenyatta University, unpublished).

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2nd ed.). Nairobi, Kenya: Oxford University Press.

Warnitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi*. Focus Publishers.

Wamitila, K. W. (2004). *Kamusi ya tashbihi, vitendawili, milio na mishangao*. Nairobi, Kenya: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. W. (2008). *Kichocheo cha fasihi simulizi na andishi*. Nairobi: Focus Publications.

Wendo, H. F. (2025). Maudhui katika ukungwi katika nyimbo teule za taarab. *EANSO*, *8*, 119–132. https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3347

Waziri, M. M. (2016). Kuchunguza dhima za nyimbo za Singo katika kijiji cha Uzini Zanzibar (Master's thesis, Open University of Tanzania, unpublished).

Yonazi, E. (2019). Kuchunguza usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu (Master's thesis, Open University of Tanzania, unpublished).